Ruvu wilayani Same, mkoani Kilimanjaro, jana wenye lengo la ...
PICHA: MARY MOSHA

NIPASHE UK 12.

# Wafugaji waelezwa umuhimu kutunza ardhi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
SIMANJIRO

WAFUGAJI wilayani Simanjiro mkoani Manyara, wameelekezwa kuanzia mwaka huu kutunza ardhi na kujiepusha kuiuza ili iwasaidie watoto miaka ijayo.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kupitia Wilaya ya Simanjiro, Lenganasa Soipey, aliyasema hayo jana kwenye harambee na uzinduzi wa kwaya ya Sayuni KKKT Mtaa wa Oloshonyokie Naisinyai na kufanikisha kupatikana Sh. milioni 12.5.

Aliitaka jamii ya wafugaji isiwe na tamaa ya kuuza ardhi kwa watu wengine kwa kuwa eneo walilonalo ni dogo na ni urithi wa watoto wao.

"Msithubutu kuuza ardhi yenu kwa shilingi, hii ardhi ina thamani kubwa mno muitunze kwa ajili ya watoto wenu kwani watakuja kunufaika nayo miaka ijayo," alisema Lenganasa.

Katika harambee na uzinduzi wa kwaya hiyo zilipatikana Sh. milioni 12.5, taslimu ni Sh. milioni 9.7 ahadi Sh. milioni 2.6 na dume moja la ng'ombe.

Lenganasa na mke wake walitoa mchango wa Sh. milioni 2.6 kwa ajili ya kuiunga mkono kwaya hiyo.

Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM Taifa kupitia Wilaya ya Monduli mkoani Arusha, Siria Saibuli, alichangia Shilingi milioni mbili na kuisihi jamii kuendelea kumchangia Mungu.

"Unapotoa sadaka kwa Mungu ni kama umemkopesha hivyo tuendelee kuwa na moyo wa kutoa ili tufanikiwe kwenye mipango yetu ya maendeleo ya ufugaji, kilimo na madini," alisema Siria.

Katika harambee na uzinduzi huo kwaya mbalimbali za kutoka Mkoa wa Manyara na Arusha, zilishiriki kuwaunga mkono kwaya ya Sayuni kwa kuinjilisha nyimbo tofauti.

zo wa kampeni aliyoizindua ya kampeni ya 'Soma na Mti' kwa tulifanikiwa kupanda 800,000 mu nyingine.

NIPASHE UK 22.



Mkurugenzi wa Uvuvi, Emmanuel Bulayi (katikati), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani), kukanusha kuhusu taarifa zilizosambaa kuwa serikali imetoa agizo la kusitishwa kwa matumizi ya taa za sola katika uvuvi wa dagaa kwenye Ziwa Victoria, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Uendelezaji wa Raslimali za Uvuvi, Didas Mtambalike na Mteknolojia wa Samaki, Masui Munda. **PICHA: MBARAKA KAMBONA**

CamScanner

# Government clarifies use of solar powered lamps in Lake Victoria

THE GUARDIAN Page 4

By Guardian Reporter, Dodoma

THE government has clarified that it hasn't halted the use of solar powered lamps during sardines (dagaa) fishing in Lake Victoria and called on fishermen to continue with their activities by adhering to the set laws and regulations.

According to the director of fisheries at the Ministry of Livestock and Fisheries, Emmanuel Bulayo, the government hasn't banned the use of the solar lamps but it emphasizes the fishermen to adhere to set laws and regulations when conducting their activities.

Addressing reporters during the weekend here, Bulayi said in supervising protection of fishery resources adheres to the National Fisheries Policy of 2015, Fisheries Act no 22 of 2003 and its regulations of 2009 and their amendments of 2018, 2019, 2029 and 2022.

"So, on sardines fishing, there are rules and regulations that need to be adhered to by fishermen, and these are found in the regulation number 66 of Fisheries Regulations of 2009 and their amendment on the use of solar powered lamps in fishing," he clarified.

He clarified that the government through the Tanzania Fisheries Research Institute (TAFIRI) conducted a study on all solar lamps used for fishing, including those that are run by motorcycle batteries and those that use kerosene and then recommended solar lamps as the best lights that should be used in fishing.

"We then approved that fishermen should use solar lamps in their boat that do not exceed 90 watts which means that each lamp should not exceed 10 watts, this is where fishermen should be very careful and stop violating the set rules and regulations," he explained.

Bulayi said the research findings have confirmed that motorcycle batteries that use 'lead-acid' cause negative impacts to the environment and affect the lake's ecology.

He said: "The government hasn't issued any order to limit the use of solar lamps as it is claimed by many. However, during the stakeholders meeting held in November 2022 in Mwanza Region, apart from other issues, it discussed this issue where it was reported that some fishermen were misusing the lamps, something which goes against sustainable fishing rules."

According to him, the meeting agreed that more education should be given to fishermen on the proper use of the solar lamps and the resolution has started to be implemented and will continue to reach more fishermen.

He further urged all fishermen in Lake Victoria and the general public to ensure that they continue with their activities but by only using friendly tools that have been approved by authorities as well as adhering to the country's laws and regulations.

On tax exemption in fishing tools, Bulayi said the government has a transparent system on the reliefs and subsidies where he called on solar lamp importers and traders to adhere to the current tax procedures.

He said the government will continue creating a conducive environment to promote sustainable fishing as well as attracting stakeholders to invest in various opportunities in the fisheries sector.

# DODOMA NEWS

From DAILY NEWS Reporters in Dodoma

DAILY NEWS Page 4.




GR
wi
gio
ove
the
wi
the
say
ma
los

go
3b
tio
wi
at
H
ea
m
to
th
cr

T
d

*DIRECTOR of Fisheries, Emmanuel*

**KAZI**

Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega ambaye ni mbunge wa Mkuranga akizungumza na wananchi wa jimbo hilo wakati wa mkutano wa kufunga mwaka 2022 ambao aliutumia kuelezea mambo yaliyotekelezwa na Serikali katika kipindi cha mwaka 2022, mkoani Pwani juzi. Na Mpiga Picha Wetu



CamScanner

Mtafungwa ameonya Mwanza. ... wa kudhibiti viwavi jeshi. ... ya mazao yanayokidhi vigezo ... sha kuchanganya mazao na ... na husafiri kwa njia ya upepo.

HABARI LEO UK 15.

# *Wavuvi wa dagaa Ziwa Victoria wapewa faraja*

**Na Mwandishi Wetu, Dodoma**

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema haijatoa agizo la kusitisha matumizi ya taa za umemejua katika uvuvi wa dagaa kwenye Ziwa Victoria ifikapo Januari Mosi, 2023, huku ikiwataka wavuvi kuendelea na shughuli zao kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayosimamia shughuli za uvuvu nchini.

Kauli hiyo ilitolewa na Mkurugenzi wa Uvuvi, Emmanuel Bulayi wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma mwishoni mwa wiki.

Alisema usimamizi wa rasilimali za uvuvi nchini unazingatia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015; Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya Mwaka 2003 pamoja na Kanuni zake za Mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2018, 2019, 2020 na 2022.

Aidha, kwa upande wa uvuvi wa dagaa vigezo na masharti ya uvuvi huu yapo katika Kanuni ya 66 ya Kanuni za Uvuvi za Mwaka 2009 na Marekebisho yake kuhusu matumizi ya taa za sola katika shughuli za uvuvi.

"Wizara kupitia mkutano wa wadau wa sekta ya uvuvi uliofanyika Novemba 2022 mkoani Mwanza na ulijadili suala hili na kuazimia kuanza kutolewa kwa elimu kuhusu matumizi sahihi ya taa za umemejua kwa kushirikiana na wadau.

Azimio hili limeanza kutekelezwa na ni endelevu. Hata hivyo kumekuwepo na upotoshaji wakati wa hili," aliongeza.

Bulayi alihimiza wavuvi wote hususani wa dagaa katika Ziwa Victoria na wananchi kwa ujumla kuendelea na shughuli zao za uvuvi kwa kutumia zana na njia rafiki ili kulinda rasilimali za uvuvi, ikolojia na mazingira kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Kuhusu msamaha wa kodi kwenye zana za uvuvi, Bulayi alisema serikali ina utaratibu wa wazi kuhusiana na masuala ya msamaha wa kodi na ruzuku.

"Wizara itaendelea kufuata utaratibu huo ili kuona uwezekano wa kutekeleza hoja husika. Nitumie fursa hii kuhimiza wadau wote wa suala hili wakiwemo watoa huduma wa taa za umemejua kufuata utaratibu uliopo kuhusu masuala ya kikodi," alisema.

Alisisitiza kuwa serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi na kwamba kila mdau mwenye nia ya kuwekeza katika fursa mbalimbali zinazojitokeza kwenye sekta ya uvuvi kufanya hivyo kwa kuzingatia sheria, kanuni, taratibu na miongozo iliyopo.

Aidha, alifafanua kuwa serikali kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) ilifanya utafiti kwa kutumia taa za aina zote zinazotumika kwenye uvuvi husika, ikijumuisha na zile zinazoendeshwa na betri za pikipiki na zinazoendeshwa na mafuta ya taa (karabai) ambapo ilipendekeza kutumika kwa taa za umemejua zenye jumla ya Watt 90 kwa chombo cha uvuvi, kwa maana ya kwamba kila taa moja isizidi Watt 10.

"Taarifa za kitafiti zimethibitisha kwamba betri zenye kutumia teknolojia ya 'lead-acid' (betri za pikipiki) zinasababisha uchafuzi wa mazingira, hasa zinapotumika vibaya na kutupwa kwenye maji, hivyo kuwa na uwezekano wa kuharibu ikolojia na mazingira ya ziwa," alibainisha.

Bulayi aliwahimizia wadau wa uvuvi kuendelea kufanya uvuvi endelevu na kwa wavuvi wa dagaa kuzingatia sheria zilizopo ili kuepuka uharibifu wa mazingira, athari kwa bioanuai na ikolojia kwa mazalia ya samaki na mazingira kwa ujumla.

CamScanner

# KANDA YA ZIWA
Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kagera





Mkurugenzi wa Uvuvi, Emmanuel Bulayi (katikati) akizungumza na waandishi wa habari kuhusu taarifa zilizosambaa kuwa serikali imetoa agizo la kusitisha matumizi ya taa za sola katika uvuvi wa dagaa kwenye Ziwa Viktoria. Kushoto ni Kaimu Mkurugenzi Msaidizi anayeshughulikia Uendelezaji wa Raslimali za Uvuvi, Didas Mtambalike. Kulia ni Mteknolojia wa Samaki, Masui Munda.(Picha na Wizara ya Mifugo na Uvuvi).

## Wataalamu wa afya waonya matumizi dawa ya 'laxactive'

Na Abela Msikula, Mwanza

WATAALAMU wa afya wameonya matumizi holela ya dawa za 'laxactive' kwa ajili ya kulainisha choo, wakasema ni mojawapo ya chanzo cha kuathiri mfumo wa chakula.

Wanasema zinapotumika bila maelekezo ya mtaalamu, zinalazimisha maji kukusanyika katika matumbo kwa dharula, kutoka kila pembe ya mwili ili kusaidia kulainisha choo, hatimaye kumfanya mgonjwa aharishe.

"Kuharisha kwa kasi ndiko kunakoathiri mfumo wa chakula," Muuguzi Msaidizi katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mwanza, Paschael John, aliliambia HabariLEO mwishoni mwa wiki.

Naye Mganga Mfawidhi wa Sekou Toure, Bahati Msaki, aliunga mkono hoja kwa kuwataka wananchi kuwasiliana na wataalam kabla ya kutumia dawa.

Akasema, mfumo mmoja katika mwili wa binadamu unapoathirika, mingine yote inavurugika na kusababisha matatizo kiafya.

Mfano, watalaamu hao wanasema, dharula ya kukusanyika kwa maji katika matumbo inasababisha sehemu zingine za mwili, ikiwemo figo, kupungukiwa maji na hivyo kusababisha uwepo wa mawe (kwenye figo).

Kadhalika maji yatapungua katika mfumo wa kutoa taka mwili nje, hali inayopelekea mkojo kubadilika rangi na kuwa wa njano, huku ukitoa harufu kali, alisema.

Walisitiza kuwa mwenye matatizo ya choo kigumu kuwasiliana na wataalamu, kwani zipo njia za asili za kutatua changamoto hiyo bila kutumia dawa.

Mojawapo ya njia asili ni kutokula chakula kigumu na kikavu, pamoja na kunywa maji ya kutosha, si chini ya lita mbili kwa siku (saa 24) au lita 1.5 kwa saa 12.

"Lakini pia ni lazima kila mlo uwe na mbogamboga pamoja na matunda ya kutosha, ili kurahisisha mmeng'enyo na hivyo kulinda mfumo mzima wa chakula," alisema muuguzi John na kuongeza:

"Wanajamii wasile chakula na kunywa maji kwa wakati mmoja, kwa sababu maji yanapenya haraka kwenye matumbo na kuzuia mmeng'enyo wa chakula".

Maji yanyweke nusu saa baada ya chakula, na kwa yule mwenye hofu ya kukabwa (na chakula), atumie matunda yenye asili ya maji, kama vile matikiti maji na matango.

Alishauriwa zaidi kwamba mitindo hatarishi ya maisha pia iepukwe kwani ni moja ya chanzo cha kuathiri mfumo wa chakula, kupitia hasa unywaji pombe uliokithiri pamoja na ulaji wa vyakula vyenye asidi/vichachu.

Pia vyakula hivyo na pombe vinapoingia tumboni hukwangua ute uliopo kwenye kuta za matumbo, ambao kazi yake ni kusaidia chakula kuteleza na kuelekea kunakostahili katika mwili wa binadamu.

Kadhalika ulaji wa vyakula vichachu uliopitiliza huathiri asidi asili anayozaliwa nayo binadamu katika matumbo, ambayo kazi yake pia ni kusaidia mmeng'enyo na vilevile kuua bakteria wanaoingia tumboni, hasa pale mlaji anaposahau kunawa mikono kabla ya kula au kuosha chakula.

## Mwanza yatoa chanjo za magonjwa ya mifugo

Na Nashon Kennedy, Mwanza

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi katika kipindi cha mwaka 2021/22 imetoa dawa za kuogesha mifugo jumla ya lita 4,612.25 zenye thamani ya Sh 207,551,250.

Hayo yalisemwa na Ofisa Mifugo wa Mkoa wa Mwanza, Peter Kaselle akiwasilisha taarifa ya udhibiti wa magonjwa ya mifugo juzi kwenye Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC).

Alisema dawa hizo zimesaidia kupunguza magonjwa yaenezwayo na kupe mkoani Mwanza kutokana na uogeshaji wa mifugo ambao umekuwa unafanyika mara kwa mara.

Alisema Mkoa wa Mwanza umetoa jumla ya chanjo za aina mbalimbali ya mifugo ili kukabiliana na magonjwa ya mifugo yanayohitaji mifugo hiyo kuchanjwa katika kipindi cha mwaka 2021/22, ambapo katika kipindi hicho kuku 645,678 walichanjwa dhidi ya ugonjwa wa kideri.

Aliongeza kuwa jumla ya ng'ombe 345,445 walichanjwa ugonjwa wa homa ya mapafu zikiwemo mbwa 2,341 na kufafanua kuwa biashara ya mifugo hai imekuwa ikifanyika siku tofauti katika minada 14 iliyopo mkoani Mwanza.

Alisema kwenye minada hiyo, wafanyabiashara hupata nafasi ya kuuza na kununua mifugo hiyo ambayo huchangia kuongeza uchumi wa mfugaji, mkoa na taifa kwa ujumla.

Alisema katika kipindi hicho, jumla ya ng'ombe 196,577 waliuzwa kwenye minada hiyo kwa wastani wa Sh 700,000 wenye thamani ya Sh 137,603,900,00, mbuzi 77,001 waliouzwa kwa wastani ya Sh 80,000 sawa na Sh 6,160,080,000 na kondoo 58,324 waliouzwa kwa wastani Sh 60,000 kwa kila kondoo mmoja ikiwa ni sawa na Sh 3,499,440,000.

Alisema kutokana na mauzo hayo ya mifugo Sh 852, 333,000 zimekusanywa na mamlaka za serikali za mitaa za mkoa wa Mwanza kutokana na ushuru wa soko ambapo ngombe mmoja hutozwa ushuru wa Sh 4,000, mbuzi na kondoo Sh 1000.

Kwa upande wa changamoto, alisema sekta ya mifugo inakabiliwa na uzalishaji mdogo usio na tija ikilinganishwa na mahitaji ya mazao ya mifugo hali inayochangiwa na wafugaji wengi wa mifugo kutofuga kibiashara.

"Lakini pia hawana utaratibu wa kuvuna mifugo yao", alisema

Alizitaja changamoto nyingine kuwa ni uhaba wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo hasa kwa Wilaya za Kwimba, Magu na Misugwi zilizo kwenye maeneo ya ukame.

Alisema changamoto nyingine ni ya upungufu wa watumishi, ambapo kwa sasa Mkoa una jumla ya watumishi 160 wa sekta ya mifugo ambapo mahitaji ni 589 na unakabiliwa na upungufu wa watumishi 429.